

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**

Simu: +255262963470  
Barua Pepe: [ps@mit.go.tz](mailto:ps@mit.go.tz)  
Barua Pepe: [gcu@mit.go.tz](mailto:gcu@mit.go.tz)  
Tovuti: [www.mit.go.tz](http://www.mit.go.tz)  
Nukushi: +255262963117



Mji wa Serikali, Mtumba,  
Mtaa wa Viwanda,  
S.L.P 2996,  
40478, Dodoma.

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

---

**UTEUZI WA WAJUMBE WA BODI YA WAKURUGENZI YA TANTRADE**

**12 Julai, 2021, Dodoma.**

Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Prof. Kitila Mkumbo (Mb.), kwa Mamlaka aliyo nayo kwa mujibu wa **Sheria ya Maendeleo ya Biashara Tanzania ya 2009, Kifungu cha 6(2)** na ameteua Wajumbe saba (7) wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (**TANTRADE**).

Wajumbe hao walioteuliwa kwa kushauriana na Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mhe. Omar Said Shaaban ni kama ifuatavyo:

1. Bw. Ally Senga Gugu kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara;
2. Dkt. Salim Hamad Suleiman kutoka Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda (SMZ);
3. Bi. Vumilia Lwoga Zikankuba kutoka Wizara ya Kilimo;
4. Bw. John Marato Sausi kutoka Wizara ya Fedha na Mipango;
5. Bi. Dorice John Mgetta kutoka Jumuiya ya Wafanyabiashara wenye Viwanda na Wakulima Tanzania (TCCIA);
6. Bw. Ahmed Suleiman Nassor kutoka Jumuiya ya Wafanyabiashara Wenye Viwanda na Wakulima Zanzibar (ZNCCIA); na
7. Dkt. Jackline David Mkindi kutoka Taasisi ya Wafanyabiashara wa Mbogamboga na Matunda Tanzania (TAHA).

Uteuzi wa Wajumbe hao unaanza mara moja.

**Imetolewa na:**

**Suzan C. Mshakangoto**  
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini  
Wizara ya Viwanda na Biashara